Kikao cha Sita – Tarehe 20 Oktoba, 2011

Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 86

Mafunzo ya Kijeshi kwa Wawakilishi

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Zipo taarifa kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limewaandalia programu maalum ya mafunzo ya Kijeshi kwa wabunge wake wote wenye umri usiozidi miaka 40, kwa ajili ya kupata uelewa wa mambo ya ulinzi na usalama wa Taifa letu. Aidha mafunzo hayo ya Kijeshi yanadhamiriwa pia kuwaandaa Viongozi hao kiafya, kisaikolojia na suala zima la ustawi wa nchi.

(a) Ni lini SMZ itaandaa mafunzo kama hayo kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

(b) Kwa kuwa mafunzo ya Kijeshi kwa wabunge yanatarajiwa kufanyika mwezi wa January hadi February, 2012. Kwanini Baraza haliungani na Bunge kutoa mafunzo hayo kwa pamoja.

(c) Je, Mhe. Waziri utakubaliana nami kuwa kitendo cha kuwapatia Mafunzo ya Kijeshi Wabunge na Wawakilishi kitasaidia kutoa uelewa, kujenga mahusiano na kuongeza ari ya viongozi kuitumikia nchi yao kiulinzi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 86 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, tumewasiliana na Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na imetuhakikishia kwamba mpango wa mafunzo ya kijeshi yanayotolewa kwa Waheshimiwa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni jambo la wabunge

wenyewe wameunda klabu yao inayoitwa *"Bunge Shooting Club"* ambayo inajumuisha Wabunge wanaomiliki silaha kisheria, wabunge wawindaji na wale wasiomiliki silaha lakini wanapenda mambo yakujifunza shabaha. Hivyo, kwa kushirikiana na vyombo husika ndio huandaa mafunzo ya shabaha na usalama wa matumizi ya silaha kwa wanachama wake.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar haina mpango wa kuandaa mafunzo ya kijeshi kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutokana na mazingira ya Zanzibar.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa amesema mafunzo haya ya kijeshi ni mpango wa wabunge wenyewe na sio mpango wa Bunge kama chombo, na kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba wako wabunge ambao wanamiliki silaha kisheria. Je, kuna mpango kwa Zanzibar kuwawezesha wawakilishi nao kumiliki silaha kisheria.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa sera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hairuhusu kwa wananchi kumiliki silaha binafsi hivyo bado serikali inaona ni jambo muafaka kuendelea na utaratibu huo mpaka pale itakapofikiriwa vyenginevyo.

Nam. 58

Gari za Abiria za Kiwengwa

Mhe. Asha Bakari Makame (Kny: Mhe. Kazija Khamis Kona) - Aliuliza:-

Gari za abiria za Kiwengwa nambari 117 zinawasaidia sana wakaazi wa Kijiji cha Pwani Mchangani kwa kutoa huduma ya usafiri. Kwa bahati mbaya, gari hizo hufikia Pwani Mchangani (round about) tu, badala ya kuingia katika maeneo ya kijiji hicho ambapo abiria waendao Pwani Mchangani hutakiwa kuteremka wakiwa na mizigo yao, na hivyo kupata usumbufu mkubwa.

Je, ni hatua gani zitakazochukuliwa na Wizara ili kuliondoa kabisa tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 58 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika ni kweli kwamba gari za abiria za Kiwengwa zenye *route* Nam. 117 zilikuwa zikiwasaidia sana watu wa Pwani Mchangani, lakini kutokana na huduma zao kutoridhisha wizara kupitia Idara ya Usafiri na Leseni tayari imeshaliondowa tatizo hilo kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika kwanza napenda kulikumbusha Baraza lako tukufu kwamba suala hili ni suala la biashara huria na moja kati ya hatua tunazozichukua ni kuwahamasisha

wananchi wetu na wamiliki wa magari waweze kujitokeza kwa wingi katika fursa kama hizo. Aidha, Idara ya Usafiri na Leseni tayari imeshayaruhusu magari mawili kufanya safari za Matemwe kwa kupitia *route* Nam. 118, katika makubaliano yao ni kwamba magari hayo yatapita na kutoa huduma kwa sehemu za Kandwi Pwani Mchangani hadi Matemwe kwenyewe.

Mhe. Spika lengo kubwa ni kuondoa usumbufu kwa wananchi wa maeneo yote tuliyoyataja. Hatua hii tunaamini itamaliza kabisa tatizo hili la wananchi wa Pwani Mchangani la kuteremshwa njiani huku wakiwa na mizigo yao. Pia Idara ya Usafiri na Leseni inaendelea kuzungumza na wamiliki wa magari ya Kiwengwa kuendeleza kutoa huduma za usafiri kwa maeneo yote ambayo yatapangiwa.

Nam. 91

Tatizo la Umeme Bustani ya Jamhuri Garden

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Wazanzibari wote wamekuwa wakishuhudia idadi kubwa ya watoto wetu wakihudhuria katika viwanja vya bustani ya Jamhuri Gardeni siku za sikukuu na siku za mwisho wa wiki zaidi kwa lengo la mapumziko na michezo mbali mbali. Nampongeza sana mwekezaji aliyeamua uamuzi huo kwani unasaidia watoto wetu kupata maendeleo ya afya na kiakili.

a) Pamoja na mafanikio hayo, zipo taarifa kuwa eneo hilo lipo tatizo la kukatika kwa umeme na miripuko ya mara kwa mara. Je, hilo ni kweli.

b) Kama hilo lipo, serikali haioni ni balaa kwa maslahi ya watoto wetu.

c) Mamlaka husika imetoa taaluma gani kwa wananchi kwa ajili ya kinga na huduma ya mwanzo iwapo tatizo litatokea.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 91 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo”-

a) Mhe. Spika, ofisi yangu haijapata taarifa ya kutokea tatizo la kukatika kwa umeme na mripuko ya mara kwa mara licha ya utaratibu wa mgao wa umeme unaoendelea hivi sasa. Isipokuwa tu niseme kwamba kulitokea tukio moja la taa moja pale kali sana kuripuka wakati jenereta lilipowashwa, taa ile kidogo ilileta mlio mkali sana labda ndio hiyo anayosema Mhe. Mwakilishi. Lakini tatizo hilo lilitokezea kwa lile jenereta lilokuwepo zamani lilikuwa na nguvu sana ikasababisha taa hiyo kuripuka lakini sasa tatizo hilo limesharekebishwa na limeshawekwa jenereta ambalo linakwenda vizuri.

b) Kwa vile eneo hilo ni eneo la mkusanyiko hivyo serikali itazidi kuimarisha ukaguzi ili kuona kwamba hakuna tatizo loloe litakalotokea kwa kuepusha balaa la aina yoyote kwa wananchi wake.

c) Serikali kupitia Baraza la Manispaa limehakikisha taratibu zote muhimu za kiusalama zimechukuliwa kwa kuweka mambo yafuatayo:-

i) Kuweka taa za njiani katika maeneo ya kiza kwenye eneo hilo.
ii) Kuweka milango mingi ya kupitia watu ya kuingia na kutoka ambayo inaweza kutumika wakati wa dharura. Kuna jumla ya milango 9, milango 4 ya kutokea nje bustani kabisa na milango 5 kutoka kwenye mapembea wenyewe.
iii) Kuweka usimamizi wa kutosha wa kuhudumia watoto.
iv) Kuelimisha wananchi au wazee kufuatana na watoto wao wanapotembelea eneo hilo.
v) Kuweka vyombo vya ulinzi na usalama.
vi) Kuweka uzio na
vii) Serikali itahakikisha kwamba usalama wa eneo hilo unaimarishwa zaidi kwa kuweka vifaa vya kuzimia moto, huduma ya mwanzo na kuwa na jenereta la dharura.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri amesema kwamba hakuna mripuko uliotokezea ila ni taa moja kali yenye mwanga mkubwa iliyotoa sauti, na kwa kuwa taa hiyo ni taa ya umeme na mlio huo umesababishwa na hitilafu ya jenereta au umeme.

a) Je, atachukua hatua gani kuwaelimisha wananchi kwa sababu wananchi ndio wenye hofu ya suala hili, atachukua hatua gani kupitia chombo husika ili kuwatoa hofu wananchi kwa suala hili.

b) Kwa sasa eneo hilo lina *fire extinguisher* ngapi ambazo zitasaidia kuzima moto iwapo itatokezea.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kubwa tunalofanya pale kwanza kuwaomba sana wazee au watoto wanaokwenda pale waende na wazee wao. Hiyo ni hatua moja wapo ili kama kutatokea matatizo kama haya madogo madogo basi wazee wawasaidie. Pia tutashirikiana na mwekezaji kutoa taaluma kwa vyombo vya habari kwamba pana usalama wa kutosha na hatua za dharura zipo pindipo ikitokezea tatizo lolote.

Mhe. Spika, kuhusu jibu (b) mwekezaji wa pale amefanya mpango na kikundi cha *red cross* na wapo vijana wa *red cross* wanakuwepo kila kituo kile kinapokuwa wazi. Vijana wale wanakwenda na vitu vyao vyote vya dharura vya kutoa huduma ya kwanza, pili na zana za kuzimia moto pindipo kutatokea moto wa dharura, lakini hatimae pia hata mawasiliano na wazima moto wetu wakubwa wanakuwa nayo kama litatokezea tatizo kubwa.

Nam. 49

Ukosefu wa Vitabu vya Kufundishia

Mhe. Mussa Ali Hassan - Aliuliza:-

Tunaipongeza Serikali kwa kuandaa mitaala ya kufundishia wanafunzi inayokwenda sambamba na umri wao. Hata hivyo, kumejitokeza malalamiko kuwa mitaala hiyo mipya iliyoandaliwa hususan wa madarasa ya msingi hayakuambatanishwa na vitabu au muongozo unaoonesha namna ya ufundishwaji wake.

(a) Je, Mhe. Waziri malalamiko hayo yana ukweli gani.

(b) Kama ni kweli huoni kuwa kufanya hivyo ni kutoa nafasi kila Mwalimu kufundisha anavyoona yeye inafaa jambo ambalo linaweza kusababisha wanafunzi kufeli mitihani yao ya taifa kwa kukosa muongozo sahihi.

(c) Wizara ina mpango gani wa kulitatua suala hilo muhimu ili wanafunzi wetu wapatiwe elimu inayolingana.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Makilishi swali lake Nam. 49 lenye sehemu (a), (b) na (c). Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba wizara imeandaa mitaala mipya ya msingi kwa mujibu wa sera mpya ya elimu ambapo elimu ya msingi itakuwa ya miaka sita. Mitaala hiyo imeanza kutumika hatua kwa hatua na kwa sasa imefikia hadi darasa la pili. Kabla ya mitaala hiyo kuanza kutumika rasmi walimu wa madarasa ya msingi wamepatiwa mafunzo ya namna ya kufundisha. Baada ya maelezo hayo napenda kujibu kama hivi ifuatavyo:-

a) Ni kweli kuwa mitaala mipya inatumika katika madarasa ya awali ya msingi bila ya kuwa na vitabu vya kufundishia. Hata hivyo, walimu wanaofundisha madarasa hayo wanatumia vitabu vya zamani ambavyo baadhi ya mada zinazofundishwa zimo.

b) Kukosekana kwa vitabu hakuathiri sana ufundishaji katika madarasa ya awali ya msingi kwani baadhi ya mada zimo katika vitabu vya zamani na hakujakuwa na mwanya kwa walimu kufundisha kwa anavyotaka.

c) Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kwa kupitia mradi wa uimarishaji wa elimu ya lazima inakusudia kutoa zabuni ya utungaji na uchapishaji wa vitabu vya madarasa ya awali ya msingi kwa masomo ya Sayansi, Hesabati, Kiingereza na Sayansi Jamii. Hatua hiyo inasubiri kupata kibali kutoka benki ya dunia na tunatarajia uchapishaji wa vitabu hivyo utafanyika hapo mwakani.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ahsante naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba baadhi ya mitaala hamna hivyo haoni kuwa hilo ni tatizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama ambavyo nilizungumza kwenye jibu langu mama ni kuwa kukosekana kwa mitaala mipya bado hakujakuwa na tatizo kubwa ingawa tunajitayarisha kutoa vitabu kwa ajili ya mitaala hiyo mipya. Na kama ambavyo nimezungumza walimu ambao wanafundisha tayari tumewapatia mafunzo ili waendane sambamba na mitaala hiyo mipya.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa elimu tunayoelekea ni elimu ya mabadiliko kutoka miaka minane ya msingi mpaka kufikia miaka sita. Na kwa kuwa msingi ndio utakaopelekea vijana hawa kuweka kumudu elimu yao ya siku za mbele na mara nyingi matayarisho yetu yanakuwa machache kama hivyo alivyosema katika majibu yake.

Je, ni sababu zipi za msingi zilizopelekea Wizara ya Elimu kuharakisha kutumia mitaala mipya wakati hawajapata nyenzo za kuweza kuwapa walimu ili waweze kutumia.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nataka nikubaliane nae kwamba elimu ya msingi ndio chachu ya elimu katika ngazi za elimu. Lakini niseme kwamba hatukukurupuka tu na kama nilivyoeleza awali ni kwamba tunakwenda hatua kwa hatua. Mhe. Spika, hivi sasa mtaala mpya ni kwa darasa la kwanza na la pili ambalo walimu wake tunawapatia mafunzo katika *TC* zetu zote za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, ni kwamba tayari tuna walimu wa darasa la kwanza 900 tayari wameshafanyiwa mafunzo hayo, wa darasa la pili tunao walimu tena 900 na Disemba mwaka huu walimu 450 wa darasa la tatu tutawapatia mafunzo hayo. Kwa hivyo, hatukukurupuka tumejipanga na tunawafahamu walimu wetu uwezo wao kwa hiyo tunaamini kama hakuna ambacho kitapungua katika hilo.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ubora wa elimu unategemea mitaala mizuri ya mitahani na tunashuhudia kwamba wanafunzi wengi wa kidato cha pili na cha nne wanashindwa kufaulu mitahani yao.

Je, wizara imejipanga vipi kuimarisha mitaala ya mitahani maskulini.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kwamba Wizara ya Elimu tumejipanga na moja ya mipango yetu ni hizi hatua ambazo tumechukua katika sera yetu mpya, sera hii kwa mujibu ilivyo mheshimiwa na kwa mujibu tunavyokwenda nayo na mitaala hii imeanza kufanya kazi na tutakapopata hivi vitabu basi nahakikisha kama hakutakuwa na tatizo lolote.

Nam. 92

Umuhimu wa Takwimu kwa Maendeleo

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Takwimu ni suala muhimu kwa mipango na maendeleo ya Taifa lolote duniani suala ambalo huiwezesha Serikali kutoa huduma kwa uhakika kwa wananchi wake.

(a) Je, Afisi ya Mtakwimu Mkuu Zanzibar inao wataalamu wa kutosha wa kufanya kazi hiyo.

(b) Kwanini baadhi ya Mawizara yana upungufu mkubwa wa taarifa za kitakwimu.

(c) Kama suala la Takwimu ni tatizo kwa Zanzibar, wananchi watarajie nini kwenye ajali ya MV Spice Islanders kuhusiana na idadi ya watu waliofariki, alioonekana na wale ambao hadi leo hii hawajaonekana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 92 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar inao Wataalamu wa kutosha wa kuweza kuzalisha takwimu za msingi zinazohitajika kwa ajili ya mipango ya maendeleo ya nchi yetu. Kwa sasa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu inao wataalamu 70 kwa mpango ufuatao:-

i) Wenye degree ya Pili (Master)	-	9
ii) Wenye degree ya Kwanza	-	22
iii) Postgraduate Diploma	-	5
iv) Advance Diploma	-	2
v) Ordinary Diploma	-	27
vi) Certificate	-	5

b) Mhe. Spika, ni kweli baadhi ya wizara zina upungufu mkubwa wa taarifa za kitakwimu hali hii inatokana na mambo yafuatayo:-

i) Kutokuwepo kwa mpango mkakati (*Strategic Plan*) kwa ajili ya ukusanyaji wa takwimu kwa baadhi ya sekta husika. Mpango ambao husaidia kutoa kipaumbele juu ya ukusanyaji wa takwimu muhimu kwa kipindi hsika (*periodically*).

ii) Uchache wa fedha ambazo hupunguza upatikanaji wa takwimu katika vipindi vinavyohitaji.

iii) Kutokuwepo kwa mikutano ya mara kwa mara baina ya wazalishaji na watumiaji wa takwimu (*User/Producer meeting*). Mikutano ambayo husaidia sana katika kuelewa ni takwimu zipi zinazohitajika na watumiaji kwa ajili ya kupanga mipango yao maendele.

iv) Shughuli za takwimu kutokupewa kipaumbele hivyo kupelekea sekta kutokuwa na takwimu za kutosha kwa ajili ya mipango yao ya maendeleo.

v) Kutokuwa na mifumo mizuri kwa baadhi ya sekta ya ukusanyaji wa takwimu hali ambayo hupelekea uhalisia wa takwimu husika kuwa sio mzuri.

c) Mhe. Spika, sehemu hii ya swali halihusiani moja kwa moja na shughuli za Mtakwimu Mkuu, na kwa vile Mhe. Rais wa Zanzibar tayari ameshaunda Kamati, namuomba Mhe. Mwakilishi asubiri ripoti ya Kamati.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Kwa kuwa amesema changamoto moja ya masuala ya takwimu ni kutokuwepo kwa mpango mkakati na fedha, na kwa kuwa yote haya yako chini ya wizara yake nini sasa itakuwa hatua ya serikali ili kurudisha tatizo la mpango wa mikakati na uchache wa fedha.

b) Mhe. Spika, Mhe. Waziri amekiri kwamba miongoni mwa tatizo ni udhaifu wa kutotumia takwimu kama zipo taasisi na mashirika hayaoni umuhimu wa kutumia takwimu. Je, serikali itachukua hatua gani ili kuwalazimisha watumie takwimu ili mipango inayopangwa na serikali isiende vibaya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza nimeshaiagiza Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kuzisaidia sekta *ministry* kuandaa mpango wa mkakati, ni mpango huu ndio utakaowawezesha sekta *ministry* kuelewa takwimu zipi zinazohitajika na zitolewe kwa wakati gani. Mhe. Spika, tayari nimeshawaagiza na tayari wanalifanyia kazi hilo.

Mhe. Spika, jambo la pili ni kwamba suala la fedha tumeshafanya maamuzi kwamba tunataka kuangalia sekta zote mapungufu yao ya takwimu halafu tuweze kuona kila bajeti tunasaidiana vipi sekta kwa sekta ili tuwe tuna takwimu za kutosha katika mipango yetu ya maendeleo.

Mhe. Spika, vile vile suala la utumiaji wa takwimu hii ni muhimu sana tumesema kwamba vikao vifanyike vya mara kwa mara baina ya watumiaji na wazalishaji wa

takwimu ili kuona kwamba ni takwimu zipi zinazohitajika na waweze kupata na waweze kuzitumia. Mimi ninachokishauri ni kwamba sote sisi tuwe tunatumia takwimu katika mipango yetu ikiwa ya mtu mmoja mmoja, ikiwa ya familia, ikiwa ya jimbo hata ile mipango ya taifa ni muhimu tukitumia takwimu tutapata matokeo mazuri zaidi.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Waziri ni kwamba wengi wanasema kwamba bajeti ya Zanzibar hailingani na takwimu hebu atupe usahihi juu ya hili.

b) Mhe. Waziri utaisaidia vipi serikali na nchi yetu kwa ujumla kuona kwamba vijana wetu wa miaka 18 wanapata vile vitambulisho vya Mzanzibari ili kuwekwa takwimu sawa ya vijana wetu wanaotimia miaka 18.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, ni kwamba bajeti yetu inatumia sana takwimu na kuna kile kitabu cha mpango ukikisoma kitabu kile utaona ni jinsi gani tulivyotumia takwimu kwa wingi sana, isipokuwa tofauti za kitakwimu zinaweza zikajitokeza katika taarifa na taarifa, hii inategemea zaidi takwimu ile umeikusanya kipindi gani. Lakini kwa bajeti yetu tunatumia sana takwimu na namuomba sana Mhe. Mwakilishi pale atakapoona kidogo kuna tofauti ya takwimu na bajeti yetu basi aje tushauriane ili tuweze kurekebisha kwa faida yetu sote.

Vile vile ameniomba nieleze nitawasaidiaje vijana wa miaka 18 katika suala zima la upatikani wa vitambulisho vya ukaazi. Mimi nataka niseme kwamba sheria ipo tumeipitisha katika Baraza hili msaada wangu mimi mkubwa ni kwamba tukiifahamu ile sheria na sisi tutakuwa hatuna matatizo. Lakini la pili ambalo naomba sana niwahamasishe Wazanzibari wote ni kujiandikisha pale wanapozaliwa. Hii itasaidia sana kuweza kuelewa kwamba huyu amezaliwa Zanzibar, anaishi Zanzibar, na hatimaye kuweza kupata hicho kitambulisho cha Mzanzibari. Sioni kama kutakuwa na tatizo kama sote tutaifahamu ile sheria inavyotutaka tufanye.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa swali langu nataka kutoa maelezo yafuatayo:-

Kwanza kwa dhati kabisa nataka nimshukuru Mhe. Waziri wa Afya kwa jitihada alizozichukua wizarani kwake. Mimi nimekuwa shahidi wa hayo ikiwemo kilio cha muda mrefu cha *ICU*, kimefikia hatua nzuri kwa muda huu.

Pia nikushukuru kwa dhati kabisa, pamoja na ufinyu unaoupata kutoka Wizara ya Fedha tumeziona jitihada zako za kutafuta wafadhili ili kuendesha jitihada hizi. Suala hili nilitaka kuliondoa lakini nafikiri utakuwa ushahidi wa waheshimiwa kupata kuona jitihada ulizozichukua kuhusu suala hili. Kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naomba swali langu Nam. 45 lijibiwe.

Nam. 45

Takataka za Hospitali

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:**

Kwa kuwa moja katika njia kuu za udhibiti wa taka taka za mahospitali ni kuchomwa moto kwa takataka hizo, na kwa kuwa hospitali huhitaji kifaa muhimu cha kuchomea taka taka hizo kijuilikanacho kwa jina la "*INCINERATOR*".

(a) Je, katika Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja kifaa hicho cha kuchomea taka kipo.

(b) Ikiwa kifaa hicho kipo; Je, kinafanyakazi.

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 45 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, na mimi pia namshukuru kwa kunishukuru juhudi tunazozifanya na kutupongeza Wizara ya Afya sio peke yangu pamoja na wafanyakazi wote wa wizara. Nategemea na mengine nayo vile vile tutafanya juhudi.

(a) Katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kuna *incinerator* mbili za kuchomea taka, kuna ile inayotumia umeme na kuna nyengine inatumia kuni ambayo inaitwa *demon fort*, ambayo ina sehemu ya kutupia mazalia ili yapate kuoza (*placenta pit*).

(b) *Incinerator* linalotumia kuni ndilo pekee linalofanya kazi, ila kuna tatizo kwenye bomba lake sio refu la kutosha na hivyo moshi hauendi juu kama unavyotakiwa. Hivyo ndio hali ilivyo hivi sasa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake ya ufasaha kabisa na yaliyo wazi. Hili *incinerator* linalotumia kuni unasema umekuwa usumbufu hivi sasa hospitali kwa moshi mwingi na kuharibu mazingira ya hospitali. Je, kuna mpango gani wa kulimaliza tatizo hilo haraka ili lisije kuleta madhara hospitali.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, mpango uliokuweko ni waina mbili, ni kuwapata wafadhili kama yeye akatusaidia na ili tupate *incinerator* lenye kiwango kinachotakiwa, *proforma* tulionayo sasa gharama yake ni dola sitini elfu, ambayo kwa kawaida ukibadilisha kwa pesa zetu ni kama shilingi milioni mia moja.

Mpango wa pili ni kwamba mapema mwaka 2012 kuna mradi mkubwa wa *ORIO* ambao utafanya marekebisho makubwa ya hospitali nzima ikiwemo kubadilisha ma-*incinerator* yote haya kwa kutumia kifaa ambacho wala hakitumii kuni wala umeme, isipokuwa kitakuwa kinatumia mvuke na huo ndio utaalamu wa kisasa. Hiyo ndio mipango iliyopo hivi karibuni.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kabla ya kuuliza swali langu na mimi kama alivyoatangaluia Mhe. Jaku Hashim nataka nimpongeze sana rafiki yangu Mhe. Waziri wa Afya hasa kwa jitihada zake na moyo wake mzuri kwa Wazanzibari na ilipofika pahala tulipombana katika masuala ya *ICU* kutokana na vile alivyokuwa anaumwa na nchi na uchungu wa wananchi alifika kutaka kujiuzulu mwenyewe bila ya kuambiwa na mtu. Lakini tunashukuru jitihada hizo amezichukua na sasa hivi hali inakwenda vizuri, Mheshimiwa tunakushukuru kwa jitihada hizo.

Mhe. Spika, swali langu liko hapa. Mhe. Waziri tunashukuru kwa jitihada zake na kama alivyoeleza katika mpango wa ukarabati au uboteshaji wa majengo ya Hospitali ya Mnazi Mmoja kwamba kuna utaratibu wa kuweka *incinerator* nyengine ambayo itakuwa inatumia mvuke.

Je, kuendelea *incinerator* hiyo kuiweka katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo tunajua kwamba vile vifaa vinavyochomwa vinatoa *pollution* ambayo inaweza ikasababisha madhara zaidi kwa jamii. Mhe. Waziri haoni iko haja kwa hiyo *incinerator* mpya pamoja na kwamba itakuwa inatumia mvuke isijengwe katika eneo la mbali na hospitali na makazi ya watu mfano kama maeneo ya Mpigaduri.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba tena kumshukuru Mhe. Hamza kwa kuona kwamba tunafanya juhudi zinazostahiki kubadilisha hali ya hospitali ya mnazi mmoja.

Katika swali lake la nyongeza ni azma yetu kwamba *incinerator* hiyo haitojengwa katika eneo la mji na hata hapo pengine Mpigaduri pana mipango ya kujengwa gati. Lakini tunategemea kuijenga nje kabisa pahali ambapo hapatoathiri harufu ya kile kinachochomwa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumuuliza Mhe. Waziri maswali ya nyongeza yenye kifungu a na b.

(a) Katika kile ambacho kinaleta jitihada za Wizara ya Afya zipo taarifa kwamba Mhe. Waziri kwenye safari yake ya Dubai ametiliana saini na wafadhili kwa ajili ya kujenga mtambo huu wa *incinerator* huko Hospitali ya Mnazi Mmoja na hospitali mbili Wete na Mjini Magharibi, na zote zina mitambo hiyo ya kuchomea takataka. Je, naomba kujua hilo ni kweli?

(b) Kama ni kweli mpango huo utaanza lini.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kidogo naomba kusahihisha kwamba ule mradi ambao nimeweka unaitwa *MOU* (*Memorandum of Understanding)*, ni makubaliano kati ya Jumuiya fulani ya Serikali ya Iran ambayo inajenga hospitali hizo dunia nzima na tumekubaliana waje wafanye uchunguzi na wajenge hospitali moja Pemba na moja Unguja itakayoendeshwa na wenyewe. Bila shaka kila hospitali inakuwa na *incinerator*, sasa *incinerator* hizo zitakuwa kwa hospitali hizo zitazojengwa. Hii tunayoizungumza

hapa ni *incinerator* inayohusu Hospitali ya Mnazi Mmoja na hospitali nyengine ndogo ndogo zote ambazo nazo zina matatizo ya kuchoma takataka zinazotoka hospitali.

Kwa mfano, nilipokwenda kutembelea hospitali ya Mhe. Hamza Hassan kule Kwamtipura napo pia wana tatizo hilo, taka wanazozichoma pale zinaathiri na zinachukiza wale wananchi wanaoishi jirani pale. Kwa hivyo, *incinerator* itakayojengwa itakuwa ni ya Hospitali ya Mnazi Mmoja lakini vile vile itatumika kwa hospitali nyengine kupeleka taka za aina hiyo. Kwa hivyo hivi ni vitu viwili mbali mbali.

Ni kweli tunategemea tutakapokubaliana na mkataba utatiwa hospitali zitajengwa moja Pemba Wete na moja Unguja ambayo tunaendelea kuwasiliana na Wizara ya Ardhi, Maji na Nishati kutupatia eneo. Lile la Pemba limeshathibitishwa na tumeshapata eneo na nadhani leo nikifika ofisini nakwenda kuweka sahihi barua kuwaambia wenzetu kwamba sisi tuko tayari wao waje ili shughuli za matayarisho zianze.

Nam. 60

Uwanja wa Gombani Pemba

Mhe. Nassor Salim Ali - Aliuliza:

Kwa kuwa Uwanja wa Gombani Pemba umeshafanyiwa matengenezo kwa kuwekwa nyasi bandia na kuleta haiba nzuri lakini Uwanja wa Amani bado una hali mbaya, mbali na ahadi aliyoitoa Waziri katika Kikao cha Baraza kilichopita cha kuufanyia marekebisho.

(a) Je, wizara ina mpango gani wa kuufanyia matengenezo uwanja huo katika kiwango chake cha zamani cha ubora na haiba.

(b) Je, Wizara inatoa uhakika gani kuhusu uwezekano wa kutumia Uwanja huo kwa Mashindano ya Afrika kwa zile klabu zitakazobahatika kuingia mashindano ya kimataifa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 60 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Uwanja wa Amaan kwa kipindi kirefu umekuwa ukifanyiwa matengenezo makubwa. Lengo la matengenezo hayo ni kuuweka uwanja huo katika hali ya ubora na haiba kuliko ulivyokuwa zamani. Lengo hilo kwa kiasi kikubwa limefikiwa kwani tumeweza kutandikwa *tartan* ya kukimbilia ya kiwango cha juu, jukwaa la viongozi mashuhuri liempanuliwa, ubao wa kurikodia matokeo umewekwa katika mfumo wa dijitali na maeneo wanayokaa watazamaji yameongezewa ubora wake. Kilichokosekana katika uwanja huo ni miundombinu ya uhakika ya upatikanaji wa maji na uwanja wa kuchezea kutokuwa katika

kiwango cha ubora unaotakiwa. Mambo hayo hivi sasa uongozi wa uwanja huo unayafanyia kazi.

(b) Mhe. Spika, hatua iliyofikiwa katika marekebisho hayo yanatia tamaa ya uwezekano wa uwanja huo kuweza kutumika katika Mashindano ya Kimataifa ya Klabu Bingwa Barani Afrika ambayo huanza mwezi Januari. Kwani miundombinu ya uhakika ya upatikanaji wa maji kiwanjani hapo imekamilika, kazi ya kung'olewa majani yaliyokuwa hayafai na kuondolewa udongo uliokuwa haufai kwa kuotesha majani uwanjani hapo imemalizika. Kazi iliyopo hivi sasa ni ya kujaza udongo unaofaa ambapo kwa mashirikiano na Idara ya Misitu undongo huo umepatikana kutoka kijiji cha Kitembeleni Wilaya Kati Unguja. Ni matumaini yetu kazi hiyo na ya kupanda majani yanayofaa itakamilika kabla ya wakati huo.

Mhe. Nassor Salim ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, mchezo wa mpira wa miguu una sheria zake na sheria za mpira wa miguu ni 17, sheria nambari moja ni uwanja. Sasa Mhe. Spika, Uwanja wa Amani jana mimi nilifanya ziara huko pamoja na Uwanja wa Mao-Tse-Tung wakati wanacheza mechi ya Wazee kutoka Uswiss na Wazee wa Zanzibar, kwa kweli ni aibu. Lakini Uwanja wa Amani Mhe. Spika, mmpandwa nyasi na vijana wa Magereza, nimeona pale wanapanda kama wanapanda mchicha.

Sasa swali langu Mhe. Spika, mwezi Januari kutakuwa na mashindano haya ya Klabu Bingwa Afrika pamoja na Kombe la Shirikisho. Je, Mhe. Naibu Waziri atatuhakikishia vipi ifikapo mwezi wa Januari uwanja ule kama utakuwa tayari.

Pili hayo maji aliyosema Mhe. Naibu Waziri ana uhakika gani kwamba maji yale yatapatikana pale kwa sababu lipo tatizo hilo la maji.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwanza najua kwamba yeye ni mdau na kipindi kilichopita alikuwa ni Katibu wa *ZFA*. Mheshimiwa tunakubaliana na wewe na kwa kushirikiana nawe ili kulitatua tatizo hili tutalifanyia kazi.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Uwanja wa Amani unatumika kwa shughuli nyingi na kwa kuwa unabeba mzigo mkubwa. Je, Mhe. Naibu Waziri huoni iko haja ya kujenga viwanja kwa kila wilaya hapa Zanzibar kuunusuru Uwanja wa Amani na kuuondoshea mzigo huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi, lakini kipindi cha bajeti lilikuja swali kama hili na tukajibu kwa kusema kuwa tutajenga viwanja kila wilaya na wilaya tutakazojenga ni kwa wanamichezo, lakini kuhusu swali ulilouliza la kuhusu kiwanja cha Amani ni kuhusu kuchezewa gwaride. Lakini nasema kwamba tuna mpango maalum na tumeshakaa pamoja na Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais kulitatua suala hili ili lisijelikatokea tena.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Atakubaliana na mimi Mhe. Naibu Waziri kwamba kwa Uwanja wa Gombani tusitie tama na kuwatia tamaa wananchi kwamba utatumika kwa mashindano makubwa. Na ni kwa sababu uwanja ule una matengenezo mengi na ni makubwa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe mimi napenda kusema kwamba tama lazima iwepo kwa sababu tayari uwanja umeshatiwa nyasi za bandia na karibuni tu tunamaliza *running track.* Taa zipo kama kawaida kila kitu kiko katika hali ya kawaida. Kwa hivyo, nina imani kwamba pengine mwezi wa Januari kila kitu kitakuwa kimeshamalizika, kwa hivyo msiwe na wasiwasi. Ahsante.

Nam. 50

Uwekaji wa Miundombinu eneo la Tunguu

Mhe. Mussa Ali Hassan - Aliuliza**:**

Uwekaji miundombinu ni muhimu pahala ambapo Serikali inakusudia kutoa viwanja vya makaazi ya wananchi.

(a) Kwa nini Serikali haikufikiria kuweka miundombinu muhimu ya maji na umeme kwenye maeneo iliyotoa viwanja huko Tunguu, Wilaya ya Kati, Unguja.

(b) Kwa kuwa suala hili halikutekelezwa hapo kabla Je, Serikali ina mpango gani wa kulitekeleza hili ili kuwaondoshea usumbufu wananchi wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 50 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, serikali imelifikiria na kulizingatia kwa umakini mkubwa suala la kuweka Miundombinu hiyo, lakini kutokana na uchache wa fedha kazi hiyo haikukamilika kwa kiwango kikubwa kama ilivyokusudiwa. Lakini kwa sasa serikali inaendelea kutoa huduma hizo kwa awamu na kuwafikishia wananchi wote wa maeneo hayo kadiri shughuli za maendeleo zinavyozidi kuimarika.

(b) Mhe. Spika, serikali inaendelea kuwapatia wananchi wa maeneo hayo huduma hizo kwa kuzingatia hali halisi ya mipango miji na ustawi bora wa jamii. Pia serikali inatoa msukumo mkubwa wa kuhakikisha miundombinu ya maji na umeme inapatikana katika maeneo hayo.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa maji na umeme ni muhimu sana kwa binadamu. Je, suala hili litafanyika kuanzia lini.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lengo lake ni kuwasambazia wananchi wake huduma ya maji safi na salama, kwa hiyo kadri ya hali ya fedha itakaporuhusu ndivyo tutakavyoendelea kusambaza mtandao huu wa maji safi na salama kwa Zanzibar nzima.

Nam. 81

Uzalishaji Sukari Kiwanda cha Mahonda

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Aliuliza:-

Katika kujiimarisha kiuchumi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliamua kumpa Muwekezaji Kiwanda cha Sukari Mahonda ili azalishe sukari na kutoa ajira kwa wananchi. Hata hivyo dalili zote zinaonyesha kwamba Muwekezaji huyo ameshindwa kuzalisha sukari kinyume na ilivyotarajiwa.

(a) Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Zanzibar juu ya hatma ya kiwanda hicho.

(b) Je, Serikali inaelewa kwamba Muwekezaji huyo ameshindwa kuzalisha sukari na badala yake anazalisha sukari guru kwa kiwango duni na spriti.

(c) Kuna madai kwamba Muwekezaji huyo anadaiwa zaidi ya milioni 50 za umeme na pia wafanyakazi wanadai malipo yao ya zaidi ya wiki 13. Je, taarifa hizo zina ukweli gani.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 81 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali inaelewa matatizo yanayokikabili Kiwanda cha Mahonda na hatua za kuyapatia suluhisho zinaendelea kuchukuliwa kwa hivyo basi:

a) Serikali inawaambia wananchi wa Zanzibar, hasa wanaopakana na mashamba kiwanda hicho kuwa wastahamilivu, wasivunje sheria kwa kufanya hujuma za aina yeyote kwa mali za kiwanda hicho wakati Serikali inaendelea kuyatafutia ufumbuzi wa kudumu matatizo ya kiwanda hicho.

b) Serikali inaelewa kuwa kutokana na tatizo la mitambo ya kuzalisha mvuke (*boiler*), kiwanda bado kinashindwa kuzalisha sukari, na badala yake kinazalisha sukari guru na spiriti.

c) Ni kweli kuwa kiwanda kina madeni ya umeme na ya malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi. Ukubwa wa madeni hayo ni tofauti na yaliyotajwa katika suala hili, ingawa si busara kuyataja hadharani madeni hayo kwa wakati huu tunapotafuta njia za kutatua matatizo ya kiwanda hicho.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipa fursa hii kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri kwa kuwa mwekezaji huyu inaonekana ameshindwa kuzalisha miwa kwa ajili ya sukari, wananchi hapa tunapata hasara mbili moja ni kukosa kuajiriwa na ya pili kukosa kuyatumia mashamba yale kwa ajili ya kilimo.

Je, Mhe. Waziri serikali ina mpango gani juu ya kuwasaidia wakulima kuweza kuyapata mashamba yale kwa ajili ya kilimo cha mpunga.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kweli mwekezaji mpaka sasa hivi ameshindwa kuzalisha sukari na ndio lengo la kupewa kiwanda hicho, na kweli wananchi wanakosa fursa ya kulima mashamba yale kwa ajili ya kuendesha maisha yao, na ni kweli ile adhma nzima ya kupata ajira wananchi wetu imekosekana. Lakini ni kwamba mwekezaji amepewa kiwanda kwa masharti na amepewa kiwanda kwa mikataba. Pia mwekezaji ameingiza fedha yake katika kile kiwanda na kumetokea matatizo mbali mbali, matatizo ambayo yametokea kutokana na wananchi ni matatizo mbali mbali.

Kwa hivyo, ni lazima serikali ichukue taratibu za kisheria ili kama kuachana na mwekezaji huyu tuachane kwa kisheria, tukitumia nguvu tu basi huyu mwekezaji anaweza kwenda Mahakamani akatushtaki na badala yake serikali ikapata uamuzi mkubwa wa kuja kumlipa na walipaji ni wale wale wananchi. Kwa hivyo, nakuombeni na nawasisitiza wananchi tuwe na subra serikali hilo inalijua na inayafanyia kazi usiku na mchana kuona kwamba tunatokana na mwekezaji huyu kwa salama na amani na wananchi watapata kile wanachokitaka.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a), (b) na (c).

a) Mhe. Spika, nini hasa msimamo wa serikali kuhusu uzalishaji wa sukari hapa Zanzibar inataka tuendelee kuzalisha sisi wenyewe au kwa mujibu wa utafiti uliofanyika sisi hatuna uwezo tena wa kuzalisha sukari licha ya mwekezaji huyo aliyeko.

b) Mhe. Spika, kulikuwa na matatizo ya mashamba pamoja na wananchi hasa katika ziara zetu za kipindi kilichopita tulipokuwa katika kamati, katika miaka hii miwili iliyopita kuna maendeleo gani ya kupitia huduma za wananchi yaliyopatikana kwa kumuweka huyu mwekezaji.

c) Mhe. Spika, inaelekea mwekezaji alikuwa zaidi akitegemea *machine* zilizopo pamoja na ukarabati alioufanya. Je, wizara imeona kutokana na *machine* zilizopo na utaalamu ulioko duniani inawezekana kutumia zile zile na akazalisha sukari.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, serikali baada ya kutokezea matatizo haya imeunda kamati tatu. Kamati moja ni kamati ya wataalamu,

wataalamu hawa wamefanya uchunguzi wa kutosha kuhusu suala zima la uwezo wa kiwanda kile kutoa sukari. Naomba kwamba hiki kiwanda hapo zamani kilikuwa na uwezo wa kutoa tani 6000 kwa mwaka, na wakati ule matumizi ya sukari nchini yalikuwa ni tani 10,000 mpaka 12,000 kwa mwaka. Kwa hivyo, kiwanda kile kilikuwa na uwezo wa kutoa angalau asilimia 50 ya matumizi ya sukari ya Zanzibar, sasa hivi sisi Zanzibar tunatumia tani 30,000 mpaka 36,000 kwa mwaka.

Mhe. Spika, kwa hivyo ukiangalia hata kiwanda kile kwa mujibu wa ardhi iliyokuwepo pale ambapo wakati huo ilikuwa ni hekta 6,000, ikitoa tani 6,000. kwa hivyo, hata hicho kiwanda kikizalisha sukari yote hiyo bado itazalisha sukari tani 6,000 ambapo ni sawa sawa na asilimia 10 ya mahitaji ya sukari kwa hapa Zanzibar. Kwa hivyo, serikali baada ya kupata ripoti itakayotoka kwa mabingwa wetu, basi itakaa iamuwe je ipo haja ya kuimarisha suala la sukari au tuachana nayo. Kwa hivyo, ningeomba tuwape nafasi hawa wataalamu wetu wafikishe hiyo ripoti yao serikalini ili serikali ipate kutoa uamuzi sahihi. Lakini kwa ufupi ni kwamba kwa mujibu wa ardhi ile tutaweza kutoa tani 6,000 za sukari kwa mwaka, matumizi ya sukari kwa mwaka ni tani 36,000. kwa hivyo, bado serikali italazimika tuagize sukari tani 30,000 kutoka nchi za nje.

Mhe. Spika, jambo la pili kuhusu mashamba hayo, bado hujuma mbali mbali zinaendelea za kung'oa miwa, miche na kupanda mipunga na hujuma za kulisha ng'ombe katika hayo mashamba zinaendelea kama kawaida. Tuhuma hizi zinaendelea na kwa kweli ningewaomba wananchi wajaribu kama inavyowezekana wasiyahujumu mashamba haya, kwa sababu kadiri wanavyohujumu basi ndio wanaipa serikali mzigo mkubwa sana kutatuta tatizo la kuachana na mwekezaji huyo, wanampa kichwa na nafasi ya kujitetea kwamba yeye mashamba yake yanashambuliwa. Kwa hivyo, wakiacha ushambulizi ule ndio wanaipa nafasi serikali ya kuweza kutumia sheria na kumuondoa kiurahisi.

Jambo la tatu, Mhe. Spika, inavyosemekana kwa mwekezaji ni kweli kamba mwekezaji ameingiza baadhi ya mitambo na mitambo mingine anatumia ile ile. Mimi binafsi siamini kwamba mitambo ile tena inafaa kuendelea kuzalisha sukari katika teknolojia ya hivi sasa. Kwa hivyo, naamini kabisa baada ya kumaliza ripoti yote ya kiwanda hiki, basi ripoti hiyo itapelekwa katika serikali na serikali itachukua uamuzi sahihi na suala hili naamini kwamba sote tutaridhika na uamuzi huo. Naomba tuwe na subra na tunaelekea katika hatua za mwisho tena za kumaliza taratibu hizi na mtapata jawabu muafaka hivi karibuni, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kumuuliza Mhe. Waziri maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kwa mujibu wa taarifa ambazo Mhe. Waziri anazieleza, inaonekana kwamba serikali imempa mwekezaji huyo ambaye hana uwezo wa kuwekeza katika kiwanda hiki.

(a) Swali langu liko hapa. Je, Mhe. Waziri ni vipimo gani vilivyotumika katika kumpatia kiwanda hicho mwekezaji huyo.

(b) Serikali imeunda kamati tatu ili kulipatia ufumbuzi wa kudumu tatizo la kiwanda hiki. Lakini taarifa tulizokuwa nazo ni kuwa kamati hizi tokea

ziundwe ni zaidi ya miezi mitatu iliyopita, hazijapatapo kukaa hata siku moja. Je, suala hili ni kweli.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante sana Mhe. Spika. Mwekezaji anapokuja hapa nchini mwetu akataka kuwekeza, vigezo tulivyonavyo ni vile ambavyo tumeviandaa katika mkakati wetu wa fomu zetu za *ZIPA*. Pale *ZIPA* kuna fomu maalum ambayo kila mwekezaji anazijaza ili kuonesha uwezo wake wa kuwekeza katika nchi yetu. Baada ya hapo kuna kamati maalum ya *ZIPA* ambayo inapitia fomu zile na kuangalia mjazo wa huyo mwekezaji na baadae kumchunguza uwezo wake kwa kila hali ili kuona kuwa mwekezaji huyo ana uwezo au hana.

Mhe. Spika, kwa kupitia vigezo hivyo, mwekezaji aliyeonekana anao uwezo wa kuwekeza katika mradi huo, lakini kama unavyojua mimi ni mfanyabiashara naweza kuwa leo hali yangu ni nzuri ya kifedha na kibiashara, lakini baada ya miaka minne au mitano mfanyabiashara yule akafilisika na akawa hana kitu. Hata nchi vile vile. Mfano leo Greece inafilisika, Portugal wiki hii itafilisika, Italy inafuatia, Belgium inafuatia. Kwa hivyo, masuala ya mfanyabiashara unaweza ukamfanya vigezo, lakini baada ya muda uwezo wa mfanyabiashara yule ukapungua na akawa hana uwezo wa kufanya biashara hiyo.

Kwa hivyo, mimi naamini kabisa kwamba serikali ilipomtia katika vigezo huyo mwekezaji, basi alikuwa na uwezo wa kutosha wa kufanya mradi huu na ndio maana akapewa nafasi hiyo. Lakini inaonekana uwezo wake umeshuka kwa kiwango kikubwa kutoka hapo siku aliyopewa hiyo kazi mpaka hii leo.

Jengine Mhe. Spika, ni kuhusu kamati tatu zilizoundwa. Mimi nataka nikuthibitishie kwamba kamati hizi zimefanya kazi zake kisawa sawa na kamati mbili zimeshamaliza kazi zake. Kamati ya wataalamu imeshamaliza kazi zake na nyengine imeshamaliza kazi zake. Lakini kamati hii ya tatu mimi nikiwa mmoja wapo, Mwenyekiti wetu alikuwa ni Jemedari Mhe. Ali Juma Shamuhuna huyo hapo na mwengine ni Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Abubakar Khamis Bakar na Mhe. Machano Othman Said yule pale.

Mhe. Spika, sisi wenyewe tumeshakutana tayari mara tatu, tumekutana na wananchi, tumekwenda katika kiwanda mara mbili na tumetembea bonde lile mpaka katika miwa yote. Kweli kazi iliyobakia sasa hivi katika kamati hii ni kwenda katika kiwanda kuangalia mashine moja baada ya nyengine ili tujuwe mpya ipi na kongwe ipi. Tulikwenda kiwandani, lakini bahati mbaya siku tuliyokwenda yule mkuu wa kiwanda alifiliwa, ikabidi tena tuakhirishe. Kwa hivyo, iliyobakia ni kazi ya sisi kamati kwenda kumaliza kwenye kiwanda chenyewe kuangalia mtambo upi mpya na mtambo upi mkongwe.

Vile vile katika kamati hii Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo yumo, na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora yumo. Kwa hivyo, ni kamati nzito yenye mawaziri 7, pia na Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili. Sote kwenye hiyo kamati tuna nia moja ya kuona kwamba tunaondokana na matatizo haya ya muda mrefu. Nawaomba Waheshimiwa

Wajumbe bado tuwe na subra na kamati inafanyakazi na hasa kwa uongozi wa Jemedari Mhe. Ali Juma Shamuhuna basi kamati hii ripoti yake itapatikana kwa muda mfupi unaofuatia. Ahsante sana.

Nam. 43

Meli za Uvuaji wa Samaki Katika Bahari ya Hindi

Mhe. Asha Abdu Haji - Aliuliza:-

Sisi wakaazi wa Pwani hasa Kusini Mashariki mwa Kisiwa cha Unguja, mara nyingi tunashuhudia kuwepo kwa meli ambazo zinaaminika kuwa zinavua samaki walio katika maeneo yetu. Hii ni rasilimali yetu ambayo sisi ndio hasa tunaostahiki kuitumia. Katika kutendeka kwa jambo hilo hakuna taasisi yoyote ambayo kisheria inafuatilia na kuwadhibiti wavuvi hao ili wasiendelee kutuibia rasilimali yetu hiyo.

(a) Je, Serikali haioni kuwa kuna ulazima wa kuanzisha Kituo cha Ulinzi kwa madhumuni ya kukabiliana na wezi hao.

(b) Je, kuna meli yoyote ya uvuvi ya kigeni ambayo imewahi kukamatwa ikiwa inavua au imekwishavua katika bahari yetu. Kama jibu ni ndio, ni lini na hatua gani za kisheria zilichukuliwa dhidi ya meli hiyo.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 43 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kuwa ni kweli upande wa Pwani ya Kusini Mashariki mwa kisiwa cha Unguja, baadhi ya siku huonekana meli nyakati za usiku bila ya watu wengi kuweza kufafanua kama meli hizo ni za mizigo au za mafuta ambazo ndio njia yake ya kawaida. Napenda kumjuilisha Mhe. Mwakilishi kuwa kituo cha ulinzi kipo na zinapopatikana taarifa za kupita meli hizo katika maji ya ndani, kituo cha KMKM, Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu, Mrajis wa Meli na ikibidi hushirikiana na Kikosi cha Maji cha Jeshi la Wananchi wa Tanzania, ili kudhibiti matukio yoyote mabaya yanayoweza kufanyika katika bahari yetu.

(b) Mhe. Spika, hakuna meli yoyote ya uvuvi ya kigeni kwa mwaka huu, ambayo imekamatwa katika bahari yetu kwa sababu ya kuvua kinyume na utaratibu.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza ambalo lina vifungu (a), (b) na (c). Mhe. Spika, kufanya doria kunahitaji kuwa na uwezo wa kuwa na vyombo vya kisasa vinavyoweza kuifanya kazi hiyo kwa ufanisi. Kwa kuwa wizara yako ambayo ndio yenye dhamana ya kulinda rasilimali zetu zilizoko baharini.

(a) Je, kwa sasa wizara yako ina uwezo gani wa kufanya doria?

(b) Ni mkakati gani uliopangwa na wizara yako katika kujijengea uwezo wa kufanya doria kwa nia ya kuzilinda rasilimali hizo.

(c) Unapofanya doria una mategemeo ya kukamata. Je, wizara yako ina mpango gani wa kujenga miundombinu ya kuhifadhia bidhaa watakazozikamata, pamoja na kuwa na uwezo wa wanasheria wa kuweza kukabiliana na kesi za aina hizo. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, nakushukuru. Ni kweli kufanya doria kunahitaji uwezo kwa kufanya kazi hiyo, ni kazi ngumu sana.

(a) Mhe. Spika, hivi karibu wizara yangu ilinunua chombo kinachoitwa *verse monitorial system* na imefunga katika ofisi ya mamlaka ya bahari kuu. Chombo hiki kinao uwezo wa kuweza kuziona meli zote zinazovua katika ukanda wa uchumi wa bahari kuu. Kwa kupitia chombo hiki tunaweza kufahamu ni ipi meli ambayo inavua kihalali na ni ipi meli ambayo inavua kiharamu. Tukishapata taarifa hiyo, ndio kwa kushirikiana kwa pamoja na kikosi cha KMKM na Jeshi la Wananchi wa Tanzania kuwa ni rahisi kwenda kumkamata muhalifu.

(b) Mhe. Spika, mkakati ambao tunaufanya ni kuimarisha kikosi chetu cha doria. Tumekubaliana na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kuimarisha nguvu baina ya mamlaka ya bahari kuu ya uvuvi pamoja na Kikosi cha KMKM, ili kwa pamoja kuwa na uwezo wa kuweza kufanya doria. Hivi karibuni Idara ya Maendeleo ya Uvuvi itanunua boti moja kubwa yenye uwezo na kasi kubwa ya kuweza kuzunguka mwambao wote na bahari yote kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(c) Mhe. Spika, miundombinu ambayo tunakusudia kuwa nayo ni kuweza kununua na kuweka maghala ya baridi katika nchi yetu, ili kuweza kukabiliana na hali hiyo. Pia kuweza kusomesha na kuajiri wanasheria wa kutosha ili hali ikitokea basi nchi yetu iwe na uwezo wa kupambana na hali hiyo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii, pamoja na majibu mazuri aliyotoa Mhe. Waziri, napenda nimuulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa chombo kilichofungwa kina kiwango chake, yaani *ranch* ya kuweza kutambua hizo meli, na kwa kuwa nchi yetu inahitaji kuwa na chombo cha *helicopter,* mbali ya doria lakini inaweza kusaidia katika hali ya uwokozi. Je, haoni kwamba imeshafika muda wa kuishauri serikali ikawacha baadhi ya matumizi na ikanunua *helicopter*, ili iweze kutumika katika kuulinda huo uchumi pamoja na hali ya uwokozi.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nakushukuru Mhe. Spika. Ni kweli kuwepo kwa *helicopter* kunaweza kusaidia sana shughuli za doria, lakini si jambo la kawaida kwamba

mamlaka za uvuvi katika nchi kumiliki vyombo hivi vya *helicopter* au ndege katika kufanya doria. La msingi katika nchi yetu, ziko taasisi za ulinzi ambazo zinamiliki *helicopter* na suala la ulinzi haliko chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kuna taasisi zake ambazo kimsingi tunashirikiana nazo ikitokea haja. Ndio maana Jeshi la Wananchi wa Tanzania inayo *helicopter* na Jeshi la Polisi inayo *helicopter,* zote hizo ni jukumu lao kuona kwamba ulinziwa nchi yetu uko salama na ununuzi wa *helicopter* hizo ni kwa ajili hiyo. Kwa hivyo, taasisi za ulinzi zilizo katika nchi yetu yaani Jeshi la Wananchi, Polisi na hatimaye KMKM naamini kwamba Mhe Spika, wanaweza kumiliki *helicopter* kwa ajili ya ulinzi wa rasilimali zetu za bahari katika nchi yetu.

TANGAZO

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, orodha wa shughuli za leo unaonesha kwamba hapo ndio mwisho wa shughuli zetu kwa leo hii. Lakini kabla ya kusitisha shughuli zetu kuna tangazo moja dogo lakini muhimu.

Nimeombwa niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe, kutoka Chama cha Mapinduzi kwamba mara baada ya kumaliza shughuli zetu wabaki huku, ili kufanya ile kazi ya mchujo wa uchaguzi wa wabunge wetu, ili hatimaye tuje tuwapate wale watatu bora kuja kuwaleta humu ndani Waheshimiwa Wajumbe waamuwe mmoja ni yupi ajaze hiyo nafasi iliyowachwa wazi na mwenzetu marehemu Mhe. Mussa Khamis Silima.

Kwa hivyo, mara baada ya kutoka hapa wawakilishi wa upande wa CCM tunaombwa tubaki kuifanya kazi hiyo. Kama nilivyosema kabla, hapa ndio mwishowa shughuli zetu kwa leo na hatutokuwa na shughuli nyengine wakati wa jioni. Basi tukubaliane kwamba tusitishe shughuli zetu hadi kesho tarehe 21 Oktoba, 2011 saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 4:20 asubuhi Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 21/10/2011 saa 3:00 za asubuhi)